## WMA YA BURUNGE

WMA ya Burunge ilisajiliwa mwaka 2006 na ilipewa haki ya matumizi mwaka 2007. Ina vijiji tisa[1] wanachama, ambao ni: Kakoi, Olasiti, Magara, Maweni, Manyara, Sangaiwe, Mwada, Ngolei na Vilima Vitatu. Ina takribani ya wakazi 34,000 kutoka makabila ya wambugwe, wabarbaig, wairaqw, wamaasai na Waarusha, ambao chini ya usimamizi wa African Wildlife Foundation na halmashauri ya wilaya walitenga eneo la kilometa za mraba 280 kwa ajili ya uhifadhi wa wanyamapori. WMA ya Burunge ipo katikati ya hifadhi ya taifa ya Tarangire, ranchi ya Manyara na hifadhi ya taifa ya ziwa Manyara, wilayani Babati, mkoa wa Manyara. WMA ipo katika mazingira mazuri sana kwa fursa za kiutalii. Kwa sasa, WMA ina makubaliano na wawekezaji wanne waonaendesha hoteli sita za kitalii na kitalu kimoja cha uwindaji.

## Kuhusu Mradi wa Utafiti wa PIMA

Utafiti wa faida na athari za Maeneo ya Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori (WMA) kwenye mazingira na umaskini (PIMA) ni mradi wa utafiti wa kimataifa ulioendeshwa kwa ushirikiano kati ya Chuo Kikuu cha London, Chuo Kikuu cha Kopenihageni, Chuo Kikuu cha Imperial cha London, Chuo Kikuu cha Edinburgh, Taasisi ya Utafiti wa Wanyamapori Tanzania, Kituo cha Umoja wa Mataifa cha Ufuatiliaji wa Uhifadhi Duniani, na Jumuiko la Maliasili Tanzania. PIMA ilikusanya taarifa za ngazi ya kaya kuhusu mali na hali za kimaisha kwa kutumia madodoso na kwa kuzipanga kaya katika madaraja tofauti ya ya umiliki mali. PIMA pia ilikusanya taarifa katika ngazi ya kijiji na WMA kuhusu uendeshaji wa WMA ikiwa ni pamoja na ugawanaji mapato. Taarifa hizi zilikusanywa katika vijiji 42 ndani na nje ya WMA sita zilizopo kaskazini na kusini mwa Tanzania. Upangaji wa kaya katika madaraja ya umiliki mali ulifanyika kwa kaya zaidi ya 13,500. Dodoso lilitumika kukusanya taarifa kuhusu mali na mbinu za kujipatia kipato kabla na baada ya kuanzishwa WMA, kutoka kwa wanaume na wanawake katika kaya zinazokaribia 2,000 (lengo ni kulinganisha hali ya maisha kati ya kipindi cha mwaka 2014-15, wakati wa utafiti wa PIMA na hali ilivyokuwa mwaka 2007 kulingana na kumbukumbu ya mhojiwa). Kwa kulinganisha mabadiliko ya hali ya maisha kabla na baada ya WMA kati ya vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA, athari za WMA katika maisha zinaweza kujulikana (Kielelezo 2).

## Mapato ya WNA ya Burunge

- Mapato yatakanayo na tozo mbalimbali katika WMA yanapaswa kugagwanywa kulingana na Kanuni zinazosimamia Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za jamii mwaka 2008 na 2012 (Kielelezo Na. 3).
- Mgawo wa mapato ya utalii hutolewa kwa serikali kuu (nyeusi) na kwa halmashauri ya wilaya (nyeupe)
- Mapato yanayobaki hurudishwa kwa Jumuiya inayosimamia WMA ambayo inaweza kubakiza nusu ya mapato (michirizi) na kugawanya nusu nyingine kwa vijiji wanachama (kijivu mpauko)
- Kielelezo Na 4. kinaonyesha jumla halisi ya mapato ya asasi ya kiraia ya jumuiya inayoendesha WMA, yaliyopokelewa na kugawanywa katika vijiji wanachama kwa kila mwaka, na vile vile kiasi ambacho kila kijiji kilipokea. Mapato kwa mwaka kwa kijiji yaliongezeka kutoka trakribani dola za kimarekani 1660 mwaka 2007 mpaka trakribani dola za kimarekani 9100 mwaka 2015. Mapato ambayo hayakugawanywa kwenye vijiji yalitumiwa na asasi ya kiraia ya jumuiya katika kuendesha shuguli za utawala na uhifadhi.
- Mapato yameongezeka kwa kadri muda unavyokwenda kwa sababu uwekezaji katika utalii uliongezeka na walianza kulipa ada, na pia WMA ilivutia watalii wengi.

## Ramani ya WMA ya Burunge




**Kielelezo Na. 1: Ramani ya WMA ya Burunge (nyeupe). Mipaka ya vijiji imechorwa kutokana na taarifa za kijiografia za ramani za vijiji, taarifa za pointi za kijiografia zinazonyesha mahali eneo lilipo kutoka NBS, WWF, TANAPA. Imeandaliwa na J. Bluwstein.**

## Jedwali la taarifa Muhimu: WMA ya Burunge

| | |
|---|---|
| Wilaya | Manyara |
| Vijiji Wanachama | 9 |
| Idadi ya Wakazi (sensa 2012) | 34,000 |
| Eneo | 280 km$^2$ |
| Mwaka wa usajili | 2006 |
| Jina la asasi ya kiraia | Juhibu |
| Mapato ya WMA [$], mwaka 2014/2015 | 381,835 |




**Kielelezo Na. 2: Mbinu iliyotumiwa na PIMA kuonesha mabadiliko yaliyosababishwa na WMA**




**Kielelezo Na. 3: Mgawanyo wa mapato ya ada za uwindaji wa kitalii na utalii wa picha kulingana na Kanuni za Utalii wa Picha 2008 na Kanuni za Jumuiya za Hifadhi za Wanyamapori za Jamii za mwaka 2012.**

* WMA inaweza kufanya makubaliano ya kuongeza kiwango cha ada, ambapo 100% ya kiwango cha ziada hubakia kwa WMA. ** Ada kubwa kabisa kwa nyara hutozwa kwa aajili ya uwindaji wa Tembo: Kati ya dola za kimarekani 10,000 - 25,000, kutegemea na ukubwa wa meno ya Tembo. *** Hukusanywa na serikali kuu, na baadae kugawanywa kwa WMA baada ya kukatwa kodi. Ada hizi ni pamoja na ada ya mikataba, ada ya kulaza wageni, ada ya kutembea eneo la WMA, ada ya kuingiza gari n.k.




**Kilelezio Na 4: Jumla ya mapato yaliyorudishwa kwenye WMA ya Burunge (baada ya serikali kukata sehemu yake) na mgawanyo wake kwenye vijiji wanachama kutokea mwaka 2006. Chanzo: Juhibu (2014). Viwango ubadilishaji fedha vimezingatia thamani halisi kwa mwaka husika**

## Mabadiliko ya Hali ya Maisha katika WMA ya Burunge

### Mali

- Kulingana na mitazamo ya wakazi, kaya za Burunge zilipangwa katika makundi ya 'maskini sana' 'maskini' 'kawaida' na 'tajiri' kufuatana na kiwango cha mali kwa mwaka 2014 na kumbukumbu za umiliki mali kwa mwaka 2007
- Kaya nyingi zilizokuwa 'tajiri' mwaka 2007 zimeendelea kuwa 'tajiri' mwaka 2014 (katika vijiji vyote, yaani vya WMA na visivyo vya WMA)
- Katika vijiji vya WMA kaya chache zilijiongezea mali kulinganisha na kaya za vijiji visivyo vya WMA




**Kielelezo Na. 5: Mabadiliko ya mali kati ya mwaka 2007 na 2014. Katika kila kaya 10, takribani kaya 3.5 zilitajirika na 0.5 zilikuwa maskini katika maeneo yasiyo ya WMA. Katika maeneo ya WMA takribani kaya 2 kati ya 10 zilitajirika.**

### Upatikanaji wa Maliasili na Mapato yatokanayo na Mazingira

- Katika utafiti huu, upatikanaji wa maliasili maana yake ni kiwango ambacho sheria na kanuni huzuia au husaidia kaya kupata kuni, fito, asali ya porini, vyakula vya porini n.k. kwa ajili ya matumizi au biashara.
- Mapato yatokanayo na mazingira imaaminisha mapato yatokanayo na ukusanyaji na/au uuzaji wa maliasili.
- Kwa kulinganisha na mapato yatokanayo na vyanzo vingine vya kimazingira, mapato yatokanayo na kuni, vifaa vya kujengea na samaki yalipungua katika vijiji vya WMA kati ya mwaka 2007 na 2014 (Kielelezo Na. 6)
- Upatikanaji wa samaki, kuni na vifaa vya kujengea ulipungua zaidi katika vijiji vya WMA kuliko vijiji visvyo vya WMA, ambapo takribani watu 2 kati ya 10 wanaiona WMA kuwa ndio sababu




**Kielelezo Na.6: Mapato yatokanayo na bidhaa za mazingira kwa vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA kwa mwaka 2007 na 2014.**

### Mbinu za Kimaisha

- Shughuli zinazoegemea katika mazingira (kama kilimo, ufugaji, mazao ya porini) zilichangia 75% ya mapato yote ya kaya za WMA ya Burunge na zisizo za WMA kwa mwaka 2014.
- Vijiji vya WMA vinategemea zaidi kilimo, wakati vijiji visivyo vya WMA, vinategemea zaidi ufugaji (Kielelezo Na. 7)
- Vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA kwa pamoja vilikuwa na mabadiliko ya njia za kujiapatia kipato kuanzia mwaka 2007 hadi 2014 (Kielelezo Na. 8). Mchango wa kilimo, mazao ya porini, mapato ya vibarua na biashara yalipungua, wakati mchango wa mapato ya misaada uliongezeka. Kupungua kwa mchango wa mapato ya kilimo, ufugaji, mazao ya porini na mapato ya vibarua kulionekana zaidi katika vijiji vya WMA




**Kielelezo Na. 7: Mchango (%) wa vyanzo mbalimbali kwenye pato la jumla (mwaka mzima) katika vijiji vya WMA ya Burunge na vile visivyo vya WMA kwa mwaka 2014**




**Kielelezo Na. 8: Mabadiliko ya mchango wa chanzo cha mapato kwa mwaka 2007-2014 kwa vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA**

### Ardhi ya Kilimo

- Ardhi ya kilimo inapimwa kwa kulinganisha uwiano wa idadi na umri wa wanakaya, na inaripotiwa kwa kufuata uwiano wa ukubwa wa eneo na idadi ya watu wazima katika kaya, yaani 'uwinano kwa mtu mzima' (AE)[2]

- Watu katika vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA kwa wastani wana kiwango sawa cha ardhi ya kilimo (kwa kipimo cha uwiano wa mtu mzima) (WMA: ekari 1.4 kwa mtu mzima, siyo WMA: ekari 1.5 kwa mtu mzima)
- Watu wengi wanayo ardhi zaidi ya kilimo katika mwaka 2014 kuliko waliyokuwanayo mwaka 2007

### Ardhi ya Malisho

- Vijiji vyote vya WMA ya Burunge na vile visivyo vya WMA vilikuwa na shida ya upatikanaji wa maeneo ya malisho ya mifugo kwa sasa, kulinganisha na mwaka 2007, isipokuwa kijiji cha Namalulu
- Katika vijiji vya WMA upatikanaji wa maeneo ya malisho umekuwa mgumu zaidi kuliko vijiji visivyo vya WMA
- 17% ya wahojiwa katika vijiji vya WMA wanadhani kuwa ukosefu wa maeneo ya malisho ya mifugo umesababishwa na WMA
- Katika baadhi ya vijiji, maeneo ya malisho ya mifugo, hasa kipindi cha kiangazi, ni tatizo kubwa (Kijiji cha Kakoi)

### Mifugo

- Neno 'mifugo' linamaanisha wanyama wote wafugwao majumbani. Ili kurahisisha ulinganishaji wa aina tofauti za wanyama na idadi (kama vile mbuzi, ndama na ng'ombe), PIMA inatumia kipimo kijulikancho kama 'kipimo cha mifugo'[3]
- Kwa wastani, kaya zisizo za WMA zina mifugo mingi, lakini kati ya mwaka 2007 na 2014 idadi ya mifugo inayomilikiwa na kaya ilipungua kwa vijiji vyote, yaani katika vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA (Kielelezo Na. 9)




Kielelezo Na. 9: Mabadiliko ya idadi ya mifugo (kwa kipimo cha mifugo) inayomilikiwa na kaya kati ya mwaka 2007 na 2014 kwa kulinganisha vijiji vya WMA na vile visivyo vya WMA

- Sababu kubwa zilitolewa kuhusu kupungua kwa mifugo ni ukame, magonjwa na mahitaji ya fedha
- Katika baadhi ya vijiji vya Burunge, wastani wa idadi ya mifugo (kwa kipimo cha mifugo) ulipungua, wakati katika vijiji vingine uliongezeka (Kilelezo Na. 10)
- Magonjwa yalitajwa kuwa ndio chanzo cha kupungua kwa mifugo katika vijiji vya WMA na visivyo vya WMA (vijiji vya Kakoi, Namalulu, Gidemar)




Kilelelzo Na. 10: Mabadiliko ya idadi ya mifugo (kwa kipimo cha mifugo, lakini hapa ikioneshwa kama ng'ombe) inayomilikiwa na kaya za vijiji vya Burunge kati ya mwaka 2007 na 2014

## Athari za Wanyamapori kwa Wakazi wa vijiji vya WMA ya Burunge

- Athari za wanayamapori kwa wakazi ni pamoja na vifo na majeraha kwa binadamu na mifugo, uharibifu wa mazao na mali nyingine. Matukio haya husababisha hasara kubwa.
- Kaya 6 kati ya 10 katika vijiji vya WMA vilikumbwa na uharibifu wa mazao kutokana na uvamizi wa wanyamapori mashambani katika kipindi cha miezi 12 iliyopita, ulinganisha na kaya 3 kati ya 10 katika vijiji visivyo vya WMA (Kielelezo Na. 11)
- Kuna utofauti mkubwa wa idadi ya kaya ziliathiriwa na uharibifu wa mazao katika vijiji vya WMA ya Burunge katika kipindi cha miezi 12 iliyopita: Kaya za vijiji vya Kakoi/Olasiti ziliathiriwa zaidi (Kielelezo Na. 11)
- Kaya nyingi za WMA ziliripoti ongezeko la viwango vya uharibifu wa mazao kati ya mwaka 2007 na 2014 kuliko kaya zisizo za WMA
- Viwango vya hasara ya mazao yaliyoharibiwa na wanyamapori, kwa kaya, vilikuwa vikubwa zaidi katika vijjiji vya WMA (Kielelzo Na. 12)
- Utofauti ni mkubwa kati ya vijiji vya WMA ya Burunge: Katika kijiji cha Kakoi wasatani wa mazao yaliyoharibiwa (angalau) ulikuwa ni mara tatu zaidi ya hasara katika vijiji vingine vya WMA
- Aina ya wanyama walihusishwa na uharibifu wa mazao ni tembo na pundamilia
- Idadi ya tembo na wakazi imeongezeka kadri miaka inavyokwenda (Kielelezo Na 13)
- Kwa kadri idadi ya wakazi na wanyamapori inavoongezeka katika eneo hili, mogogoro kati ya binadamu na wanayamapori inaongezeka zaidi
- Sababu nyingine, kama wanyapori wanavyozidi kuwazoea watu na kuacha kuwaogopa, au kupanda aina mpya ya mazao ambayo wanyamapori wanavutiwa nayo, kunaweza kuongezea misuguano kati ya binadamu na wanyamapori.




Kielelezo Na. 11: Wastani wa uwiano wa kaya za WMA (56%) na zisizo za WMA (27%) zilizokumbwa na uharibifu wa mazao kutokana na uvamizi wa wanyamapori mshambani katika kipindi cha miezi 12 kabla ya utafiti




Kielelezo Na. 12: Wastani wa hasara iliyotokana na uharibifu wa mazao kwa kaya katika vijiji vya WMA na visivyo vya WMA. Angalizo: Kiwango cha hasara kimekokotolewa kutokana na makadirio ya eneo lililoharibiwa, uzalishaji wa mazao, na makadirio ya pesa za mauzo ya mazao




Kielelezo Na. 13: Kukua kwa idadadi ya wakazi (mraba, mstari wa kulia) na tembo (almasi, mstari wa kushoto). Chanzo: TAWIRI (2014), HDIC (2010), WWF (2014).

## Hitimisho

Vikwazo katika upatikanaji wa ardhi, maji, kuni na rasilimali nyingine unaathiri wakazi wa WMA ya Burunge. Mifugo, kilimo na mazao ya porini vilichangia robo tatu ya mapato yote ya kaya za WMA na zisizo za WMA kwa mwaka 2014. Kwa wastani, mifugo inayomilikiwa na kaya za WMA na zisizo za WMA ilipungua ikilinganishwa na mwaka 2007. Ardhi ya kilimo haikuwa na mabadiliko tangu mwaka 2007. Upatikanaji na matumizi ya kuni na vifaa vya kujengea umepungua zaidi katika vijiji vya WMA kuliko kwenye vijiji visivyo vya WMA, na upatikanaji wa ardhi ya malisho kwa sasa umekuwa mgumu zaidi katika vijiji vya WMA ikilinganishwa na vijiji visivyo vya WMA. Aidha, migogoro kati ya binadamu na wanyamapori imeongezeka katika ukanda ambao idadi ya tembo na wakazi imeongezeka. Vijiji vya WMA hupoteza zaidi mazao kutokana na umvamizi wa wanyamapori mashambani kuliko vijiji visivyo vya WMA. Licha ya mazingira na hali kuwa tofauti katika vijiji wanachama, vijiji vyote vya WMA vinapokea kiasi sawa cha fedha kutoka katika ofisi ya WMA na hakuna fidia kwa hasara zinazosababishwa na shughuli za uhifadhi. Mapato ya vijiji kutokana na utalii katika WMA yanapungua kwa sababu sehemu ya mapato huchukuliwa na serikali kuu na halmashauri ya wilaya, na kutokana na asasi ya kiraia ya jumuia ya Burunge kutumia sehemu ya mapato katika kugharamia shughuli za utawala na uhifadhi. Wanajamii wana ushawishi mdogo juu ya jinsi mapato yanavyotumiwa na asasi ya kiraia ya jamii na jinsi yanavyogawanywa miongoni mwa vijiji wanachama. Asasi ya kiraia ya jamii kwa sasa inatoa kipaumbele zaidi kwenye mipango ya kupambana na ujangili, bila kuimarisha mipango ya kukabiliana na migogoro kati ya binadamu na wanyamapori na ulipaji wa fidia. Mmoja kati ya wawekezaji kwenye WMA (Chem Chem Safaris) anashikilia maeneo makubwa ya ardhi ya kijiji na kusababisha kukosekana au upatikanaji mdogo wa ardhi kwa wanajamii. Mivutano juu ya ugawanaji usio na usawa wa faida na gharama za uhifadhi unaendelea kuchochea migogoro na matukio ya vurugu kati ya askari wa Burunge, walinzi binafsi wa Chem Chem na wakazi wa WMA ya Burunge.

## Kumbumbuku Rejea

[1] Minjingu ni kijiji mwanacha wa kumi, lakini hakijawahi kuutambua uanachama wake na kinakataa kupokea mapato kutoka ofisi ya WMA. Mgogoro kuhusu uanachama wa kijiji cha Minjingu kwa sasa upo mahakamani.

[2]Katika matokeo haya, ardhi ya kilimo imeainishwa na idadi ya watu katika kaya, jinsia na umri, kwa sababu wanaume, wanawake, na watoto wa umri tofauti huhitaji kiwango tofauti cha chakula, na hivyo ukubwa sawa wa ardhi humaanisha uwezo tofauti wa kutosheleza mahitaji kwa kaya mbalimbali. Kwa kutumia mfumo sanifu, tunawajumlisha wanakaya na kuwaweka katika kipimo cha 'uwiano wa mtu mzima' (AE), ambacho ni rahisi kulinganisha umiliki wa ardhi ya kilimo na mahitaji kwa kaya

[3]Kama ambavyo PIMA imetumia mfumo sanifu wa uwiano wa mtu mzima (AE), tunatumia 'kipimo cha mifugo' ili iwe rahisi kulinganisha makundi ya mifugo yanayoundwa kwa aina na ukubwa tofauti wa mifugo na mahitaji yao tofauti ya chakula. Kipimo kimoja cha mfugo ni sawa na ng'ombe mmoja mkubwa wa kilo 250kg. Mbuzi au kondoo kwa mfano, anahesabiwa kuwa sawa na moja ya kumi ya ng'ombe.

## Shukrani

PIMA inawashukuru wakazi wa vijiji vya Kakoi, Olasiti, Magara, Maweni, Manyara, Mwada, Ngolei, Sangaiwe, Magugu, Gidemar, Kisangaji na Namalulu, na Jumuiya ya Hifadhi ya Wanyamapori ya Burunge kwa kushiriki katika utafiti huu. Mradi wa utafiti wa PIMA umefadhiliwa na ESPA: Mpango wa Utafiti wa Mazingira na Kuondoa Umaskini. ESPA inaendeshwa kwa pamoja na Shirika la Misaada ya Kimataifa la Uingereza (DFID), Baraza la utafiti wa Mazingira (NERC) na Baraza la Utafiti wa Uchumi na Jamii (ESRC). Kwa maelezo zaidi tembelea tovuti hii: www.ucl.ac.uk/pima

Jarida hili limeandaliwa na S. Funk kutokana na takwimu zilizokusanywa na mradi wa utafiti wa PIMA. A. Keane, M. Reinhardt Nielsen, J. Friis Lund, J. Bluwstein and K. Homewood kwa pamoja waliandaa mbinu za kukusanya, kuchambua na kutafsiri takwimu za PIMA. J. Olila aliongoza kikundi cha wakusanya takwimu. M. Msuha and N. Burgess walihusika na takwimu za wanyamapori.

## Marejeo

Health and Development International Consultants (HDIC) (2010): Socio-Economic Baseline Studies in Selected Wildlife Management Areas under the Financial Crisis Initiative/Cash-for-Work Program Burunge WMA Report. Final Report. With assistance of USAID, WWF, AWF. Edited by HDIC. Dar Es Salaam, Tanzania.

Juhibu (2014): 2014 Juhibu Financial Report (AA). With assistance of F. Moyo accessed in Burunge AA office in 2015.

TAWIRI (2014): Elephant population estimate in Tanzania. Countrywide African Elephant Survey 2014.

WWF (2014): Tanzania's Wildlife Management Areas, 2012 Status Report.

**Mawasiliano:** K. Homewood, Chuo Kikuu cha London, Idara ya Anthropologia. k.homewood@ucl.ac.uk